JUA
GAZETI LA MAENDELEO
Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 22 - Toleo la 450

# Moto umewaka mjini Kananga

Mabadiliko ya pesa yaliyojulishwa na kuendeshwa hata sasa nchini Zaïre yaleta matukio ambayo kila mkaaji na raia azungumuzia kila mara akikutana na mwenzie. Ni kweli jambo la kuunga mkono ikiwa serkali ingelichukua mipango yote ya kuinurisha pesa hizo na kupinga watu wa nia mbaya hawapendi uchumi wa nchi yetu uongoke.

Tangu hapo serkali ya muungano wa raia inayoongozwa na waziri mkuu Faustin Birindwa ilipofahamishwa kuweko mabadi-liko ya feza, kelele kasikika pande zote. Watu kazaa kama vile wapinzani, miradi ya maendeleo na mazehebu ya kidini mamoja kashawishi watu kutokupokea feza hizo mpya.

Kulingana na jambo kama lile la kukataa feza hizo ikaonekana kama wakaaji wa vijijini ambao wategemea wakuu wa kidini *na miradi na pia mashirika ya akiba na mikopo* kajikuta kuwa *mbele ya kitendawi-li* ambacho wasijue lakufanya. Kitendawili hicho kilihusika na kukamata azimio la kuchukua ao kukataa feza mpya. Huko mda ukipita mno. Pahali wakaaji wangekuwa na muda wa mwezi moja kwa kubadili kwa utulivu feza zao ilionekana tu kama juma mbili ndizo zilizo baki kwa baazi ya wanamiradi, makanisa na wale waliokataa kukubali. Kufuatana na jambo lile ilionekana kuwa uchumi wa wakaaji vijijini kazorata kwa hali mbaya sana na kusa-babisha bei kupanda kiasi cha ajabu. Yaonekana kama maskini hao wa vijijini wataanza upya maisha mengine kwa yale walionayo.

Na yasemekana kuwa huko vijijini watu hujibadilishia vitu (troc) kwa ajili ya kununua. Wale walio jichungia mali manyumba-ni walia na kusaga meno kuona idadi yao ya pesa kubwa haitatole- wa kwenye mabenki. Bwana Frederic Mwene Lwata Isonga Mpala aliye katibu mkuu wa serkali ya waziri mkuu Birindwa katika mkutano wake na muungano wa wapasha habari kafahamisha kuwa huko mjini Kinshasa shirika moja fulani kajiwekea pesa katika ma "containeurs" kazaa. Na hapa Bukavu yasemekana kuwa mtu moja kajiwekea nyumbani mwake kiasi cha miliari mia tano elfu ya Zaïres.

Na si hao tu na wengineo ambao baada ya kusikia mabadiliko ya pesa kapendelea kuuza vitu kwa bei yote katolewa na kuleta mripuko wa bei kiasi cha ajabu kwenye masoko na maduka. Baada ya siku kama vile ine hivi, bei kapunguka kidogo ila baadaye tena yaendelea kupanda.

Kulingana na feza hizo mpya ambazo zatakiwa na kila moja, matatizo ni kuona bado benki hazijatoa noti zile za kidogo na vichele ambazo zaitwa makuta 50, 10, 1 na wengine wajiruhusu kupanga bei kadiri watakavyo.

Habari zinazo aminiwa lajulisha kama mjini Kananga, katika jimbo la Kasaï ya magharibi, askari-jeshi wa kundi 223 kakasirika kuna raia wamejiruhusu kukataa pesa ya zaire mpia. Tarehe 29/11/93 askari-jeshi hao wameharibu mji wa Kananga na kuiba madukani, sokoni na nyumbani mwa wakaaji hata kufikilia kuuwa watu watatu. Kati ya watu hao kafari kwa risasi Padri mmoja mbeleji kwa kiburi yake yakukataa kushika sheria ya inchi yetu, akiwaza Zaïre ingali katika koloni mwa wabeleji.

**Mutungwa Abandelwa Phély**

# Rubenga wa Idjwi amefariki, lakini !

Kufuatana na kifo cha mwami Rubenga kilichotokea *kisiwani* Idjwi mnamo siku zilizopita, wasimamizi wa makundi fulani fulani, wakuu serkalini na wa asili na wakaaji wengi wa mtaa ule kaomboleza na kutoa maoni kazaa kuhusu ayati Rubenga.

Ndugu Ntambuka Balekage aliye mwami kwa jumla wa mikoa hiyo ya Idjwi "nord" na Idjwi "sud" tuliyehojiana naye katufahamisha kuwa muungano wa Bahavu uliyosimamiwa na mwalimu Charles Magabe kanena yakuwa ayati Rubenga alikuwa na ujuzi mwingi, alipendelea kupokea mtu wowote na kutendea watu mema pia kujua haki yao. Mwami huyo kawatetea raia waliokuwa wakigandamizwa na kiongozi wa mtaa moja aliyekuweko Idjwi. Kwa hali ya ujuzi wake, mwami Rubenga kamsimika mwanae kiasili tangu mwaka wa 1974 ingawaje binafsi alikuwa akiishi na kuwa na nguvu ya kuongoza. Muungano wa bahavu kasisitiza na kusema *ikiwa* "Bami" wote wangeiga mfano wake ingelikuwa furaha ya raia.

Kwa ngambo ya tume lihusikalo na haki na amani (commission justice et paix) ambalo wajumbe wake hawakuonekana lakini iliyotetewa na bwana Bifuko kajulisha kuwa mwami Rubenga kafariki na miaka 83 akiwa mzazi wa watoto 37. Yeye alikuwa mpatanishi ambaye kaunganisha mikoa ile mbili. Alianza kutumika kazi ya barabara toka Goma hadi Bukavu mpaka hapo hakuwa na neno lolote hata alipotoweka ulimwenguni. Pia alionekana kuwa mshauri wa wenzio na raia wake.

Kwa niaba ya Bami wote wa Kivu ya Kusini, mwami Ngweshe kasisitiza na kusema kúwa ayati Rubenga kaishi na amani na watu wote hata hivyo walipokuwa wakihusiana kwa njia ya vibarua. Pia mwami Ngweshe kaomba kwa mrizi aliyechukua madaraka kufuata mfano wa babae. Kwa upande wa wakaaji wa Idjwi, maoni yao yalikuwa kama yale ya ndugu Bifuko.

**Mutungwa Abandelwa Phély**

## Neno la wasomaji

# Itombwe yabaki nyuma

Itombwe, ni moja ya mikoa inayounda mtaa wa Mwenga jimboni mwa Kivu ya Kusini. Mkoa huo baada ya kukabiliwa na vita vya wahuni yapata miaka ishirini na tano hivi, waendelea kubaki nyuma kimaendeleo na serkali vyaweza kuendesha eneo hilo.

Wanainchi wenyewe waweza kujitoa na kufanya jambo la muhimu lakini hawajali na washugulika tu na ufugaji na uchimbaji wa madini. Ingelikuwa vema hata kwa uchungaji ao kwa ufugaji wao watengeneza kiwanda cha dibini (fromage, beurre) kitakachowapa kazi vijana na kuepuka uamiaji wa mjini mkuu (exode rural). Hiyo ni shida kubwa.

Kwa ngambo ya makanisa, waweza kuendelesha Itombwe lakini hawana ushirika kati yao na kati ya waumini wao. Ila twaweza kusifu kanisa la kimethodisti ambalo lina vyumba vya kutunza wagonjwa sehemu mbalimbali pa Itombwe. Pia kanisa la CELZa lajitahidi pia kwa njia hiyo na wote kwa ujenzi wa masomo.

Kwa upande wa mashirika ya maendeleo, hakuna hata mradi moja unaoweza kuonekana kazi zake pa Itombwe. Hata kama kwa majina miradi yaonyesha mengi.

Kwa ngambo ya serkali, ni sikitiko kuona halijafanya hata lolote huko Itombwe. Watu walioteswa na uhuni na vita vya wahuni wangeshurulikiwa hasa kuliko wengine. Ajabu ni kuona serkali, haina hata masomo, hospitali huko lakini ilijaribu kutoa pesa za kufungua njia ya Itombwe hadi Fizi, lakini pesa zile haziwezi kitu.

Wazaliwa wa Itombwe wangepaswa kujua kama wakingoja serkali iwafanyie vyote wajidanganya sababu Soko, mtu haiwezi tena kupatamkia. Lakini twapongeza mabwana Ngumba H.S. na Ishangulungu kwa kazi yao. Ni wajibu wa serkali na mashirika mengine kutendea vizuri, raia wanaokaa hasa vijijini.

**Msomaji wako :**
**Ngoy Waso Pene Mulenda**
**poste SNIP/DI-Mp**
**Antenne d'Itombwe**
**Mwenga**

## UHARIRI

# Ufalme wa Kristu ni ufalme wa haki na mapendo

Nchini Zaire, kutokana na kuzorota kwa siasa ya uongozi, ya kiuchumi na ya kijamii, yatezamiwa mapambano makali yapo kati ya viongozi wa makanisa na hao wa serkali. Lakini ingekuwa vema kati ya serkali na makanisa kusiweko migongano kwa kuwa wote washurulikia raia. Kwani mtu ili afikie utu wake, yafaa awe hai kimwili na kiroho.

Hapo jimboni mwa Kivu ya Kusini, baada ya viongozi wa dini katoliki kukutana na waziri wa Sheria, bwana Yusyfu Guhanika, hapa mjini Bukavu, Mzee Munzihirwa, arkiaskofu wa Bukavu kwa mda katoa maoni yake kuhusu masimulizi walioifanya.

Wandugu wapenzi,

1. Mulisikia kwa njia ya mawimbi ya anga ya kama waziri wa Uhaki alitualika kwa mkutano, tarehe 13 wa mwezi huu pa saa 10 mbele ya mchana-kati.

- Ukomo wake ulikuwa wa kutupasha kama huko Kinshasa walipokea barua za uchongezi "ya kama hapa Bukavu Kanisa katolika inawasaidia wakaaji kupinga mipango ya serkali ya leo".

2. Jibu letu ni la kuwa Kanisa haipingi mipango mizuri ya serkali. Lakini kwa amri ya Kristu sherti tulalamike kila mara ndugu zetu, wanadamu wanapoangamizwa na kukosewa haki.

Naye waziri ameturudishia ya kuwa inafaa tufanye angalisho tusifanye matendo yanayokatazwa na amri ya serkali.

Nasi tumejibu ya kuwa sherti tulalamike kama amri zinazuia mpanuko wa haki za kiini za kila binadamu.

3. Ndiyo maana leo tunalalamika juu ya ushuru unaombwa na maaskari kwa nguvu na kijeuri pa kila kizingo cha barabara kwa wachuuzi wanaoenda sokoni. Tena sokoni wanalazimishwa kutoa ushuru kwa waaskari wenyi silaha za kunyanganya baadaye kodi ya serkali kwa uchuuzi wao ! Kwa bizaa vile vile mara tatu.

4. Ndiyo maana tunawaomba pia wáamzi waende kuangalia gereza : leo waliomo vifungoni kwa makosa madogo wangaliachiliwa kufa na njaa ! Wakaaji wote wanakosa sasa chakula cha kutosha kwa jamaa yao, na misaada ya kuwatolea wamaskini.

5. Tunaomba serkali iwafunguwe wafungwa walioazibiwa kwa mambo madogo, wasifie gerezani kwa njaa, na ukosefu wa afia yoyote.

6. Tunaomba pia wafungwa wenyi kutiwa katika vijumba vya kifungo vya waaskari mbele ya kukatiwa mashtaki, wasipigwe, wapokee salamu na chakula chenyi kuletwa na jamaa zao.

Sifa ya Mungu ni mtu mzima na mwenyi heshima ya Mungu na nduguze.

**Mzee Munzihirwa**
**Mhudumu wa Kanisa ya katolika**
**Arkidiosezi ya Bukavu**

# Je, umesikia ... ?

**KUWA**, shruli za kubadili pesa kawawinisha wale walio kati ya wabadili na wanaotoa pesa mpya ambao waonekana wapenda feza mno na waitwa sasa mabwana "10 %" ao mabwana "nouveaux-Zaïres" ?

Ndugu hao walikuwa wakizunguka zunguka kando kando ya mabenki na kufikako tangu saa 11 ya asubuhi (5 heures) huko wakiorozesha vikartasi waliokuwa wakiwapa watunza hazina. Yasemekana kuwa mnamo saa za mangaribi, mabwana wale walipashwa kukutana na wanunuzi wao kwa ajili ya kujipatia hiyo 10 % ao "Commission" ambao wapenda feza hao walikuwa wakigawanyana. Kwa bahati nzuri, kitendo hicho hakikudumu sababu ya mashirika ya akiba na mikopo "Coopecs" na chumba cha akiba (Cadeza) vilivyonusurisha hali ya mambo kwa mshangao wa mabwana 10 %.

**ETI**, manunguniko na kupandishwa kwa bei mjini Bukavu na kandokando katukia kuhusu mabadiliko ya feza yaendelea kuleta hasara ? Loo ! Eti ukosefu wa vifaa na hasa njaa yawalaza wakaaji. Hum ! Eti baada ya wakaaji kukataa noti ya milioni tano ambayo kaitwa "Dona Beija", ni tangu siku kazaa watu kapinga na kutupi lia mbali kuchukua noti ya zaïre mpya 50 ambayo yaruhusiwa na kutolea na Benki kuu. Ebu ! Kwa hiyo noti, watu wamegundua kulipatia jina la "Cinquante Nani Zoba" ! Na hiyo yatokana na ukosefu kwenyi noti ya singa ya usalama na yachapichwa huko Kinshasa umbalimbali na zingine ambazo zachapwa Ujeremani.

**KWAMBA**, makamu wa liwali hapo zamani, bwana Ngoy Shambuyi Kapenzu ashtakiwa kama vile liwali wa zamani Dilingi mbele ya kuondoka mjini Bukavu kitendo haramu cha kuchukua vifaa vya makao ya kiserkali alimokuwa bila uwasiwasi na kufyatuka navyo?

Allah ! Wanaoendesha mashtaki hayo si wengine bali watumishi wa chumba cha TP/AT wakati waulizwa. Ingawa ni wao wizi wa vifaa vyatezamiwa kupeperushwa. Eti vifaa hivyo vyauzishwa na watumishi hao kwenyi soko la "Bwaki" mtaani Kadutu kutokana, wasemavyo, na kutolipwa mishahara yao ili wapate lwa sombe na ..." Kwa kuwa siku ya mwizi ni 40, makamu wa liwali wa jimbo kwa sasa, bwana Lwabanji, kaelezwa mambo hayo baada ya kupigwa bumbuazi wakati kajielekeza kwenyi makao kakabizwa ili ajionee binafsi hali ya makao hayo.